***SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR***

**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

# RIPOTI YA NNE
# YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI
# KWA MWAKA 2019/2020

**Septemba, 2020**

(Imewasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)

**YALIYOMO**

JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO ............................................... 4

MAELEZO YA MWENYEKITI ............................................................... 5

1.0 UTANGULIZI ............................................................................ 10

1.1 DIRA .................................................................................. 11

1.2 DHAMIRA............................................................................ 11

1.3 MAADILI YA MSINGI ........................................................... 11

1.4 LENGO KUU ....................................................................... 11

2.0 MUUNDO WA TUME YA MAADILI ............................................. 12

2.1 IDARA ZA TUME YA MAADILI................................................ 12

2.2 WATUMISHI WA TUME YA MAADILI...................................... 13

2.3 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI ....................................... 13

2.4 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI........................ 15

3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2019/2020 ........ 16

4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2019/2020 ........................................................................ 17

4.1 TAMKO LA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ................... 17

4.1.1 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni ........................................................................ 18

4.1.2 Uchambuzi wa Fomu ................................................ 18

4.1.3 Kutangaza Majina ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali ............................................................. 20

4.1.4 Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Taarifa za Viongozi Wasiojaza Fomu ........................................................................ 20

4.2 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ........................................ 20

4.3 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA ........................................................................ 21

4.3.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki............................................ 22

5.0 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA .......... 24

5.1 Uchambuzi wa Malalamiko............................................ 25

6.0 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA............ 26

6.1 Mikutano na Viongozi wa Umma ...................................... 26

6.2. Mikutano ya Wananchi na Wanafunzi ........................................ 27
6.3 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari ........................................ 28
6.4 Utoaji wa Machapisho na Matangazo ........................................ 28
7.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI ........................................ 29
8.0 KUWAPATIA MAFUNZO YA KITAALAM WATUMISHI WA TUME YA MAADILI ........................................ 30
9.0 KUKUZA NA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA UHUSIANO KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA ........................................ 31
10.0 VIKAO VYA TUME ........................................ 32
11.0 HALI YA MAPATO NA MATUMIZI ........................................ 32
12.0 VIKWAZO NA UTATUZI WAKE ........................................ 33
13.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2020/2021 ........................................ 34
14.0 MAPENDEKEZO ........................................ 35
15.0 HITIMISHO ........................................ 36
16.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI ........................................ 37

## JADWELI, MICHORO NA VIAMBATANISHO

### JADWELI

Jadweli Nambari 1: Idadi ya Watumishi wa Tume ya Maadili na Viwango vyao vya Elimu.......................................................................................... 13

Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu............................ 19

Jadweli Nambari 3: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020 ................................................................................................. 22

Jadweli Nambari 4: Idadi ya Malalamiko iliyopokelewa 2019/2020.............24

Jadweli Nambari 5: Mikutano ya Viongozi, Wananchi na Mabaraza ya Vijana waliopatiwa Elimu ya Kukuza Maadili ................................................. 28

Jadweli Nambari 6: Hali ya Mapato na Matumizi....................................... 33

Jadweli Nambari 7: Mchanganuo wa Matumizi kwa Mwaka 2019/2020 ......32

### MICHORO

Mchoro Nambari 1: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu............................ 19

Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020 ................................................................................................. 23

### VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.................................................................................................. 39

Kiambatanisho Nambari 2: ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA.................. 40

## MAELEZO YA MWENYEKITI

Hii ni Ripoti ya Nne ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015, kinachoeleza kwamba:

> "29(1) Mwenyekiti atatayarisha Ripoti ya Mwaka na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha husika.
>
> (2) Ripoti ya Mwaka itajumuisha maelezo kuhusu utekelezaji wa kazi za Tume.
>
> (3) Baada ya kupokea Ripoti chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais atamtaka Waziri kuiwasilisha Ripoti hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi katika kikao kijacho".

Tume ya Maadili imetimiza miaka minne tangu kuanzishwa kwake ikiwa na jukumu la kusimamia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015. Sheria hiyo imeainisha majukumu mbalimbali yakiwemo kupokea, kusajili na kufanya uhakiki wa Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma. Tume ya Maadili pia inapokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko au tuhuma za ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma, kuchunguza mwenendo wa Kiongozi yeyote wa Umma ambao unaweza kusababisha au kuchangia uvunjwaji wa maadili chini ya Sheria ya Maadili na kuelimisha Viongozi wa umma na wananchi kuhusu umuhimu wa kuimarisha na kufuata misingi ya Maadili. Kwa msingi huo, ninapenda kuelezea kwa ufupi utekelezaji wa majukumu hayo, mafanikio na changamoto zilizojitokeza.

Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu yake, Tume

ya Maadili imepokea na kusajili Fomu za Tamko la Mali na Madeni 1,620 kwa mwaka 2016, fomu 1,664 kwa mwaka 2017, fomu 1,702 kwa mwaka 2018 na fomu 2,325 kwa mwaka 2019. Ongezeko hili la idadi ya fomu zinazowasilishwa linatokana na juhudi za utoaji elimu kwa viongozi kupitia programu mbali mbali, kuanzishwa kwa taasisi mpya kunakotokana na matakwa ya kisheria na utekelezaji wa mpango wa ugatuzi uliopelekea kuanzishwa kwa nafasi mbali mbali za uongozi ikiwemo Wakurugenzi Wasaidizi na Wasaidizi Katibu Tawala. Kadhalika, idadi ya viongozi waliochelewa kuwasilisha Fomu za Tamko imekuwa ya kuridhisha kutoka 141 kwa mwaka 2016/2017, 25 kwa mwaka 2017/2018, 26 kwa mwaka 2018/2019 na 53 kwa mwaka huu wa utekelezaji 2019/2020.

Katika kutekeleza kazi ya msingi ya uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma kwa mwaka huu wa utekelezaji 2019/2020, jumla ya viongozi 135 wamehakikiwa ikilinganishwa na viongozi 38 katika mwaka 2016/2017, viongozi 103 katika 2017/2018 na viongozi 168 katika mwaka 2018/2019. Katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzisha Ofisi ya Tume ya Maadili, uhakiki huu uliwajumuisha Mawaziri na Manaibu Waziri, Makatibu na Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya Umma, Wakurugenzi, Makamishna, Wahasibu na Wakaguzi wa ndani. Licha ya Tume ya Maadili kutekeleza kazi hii, bado kuna changamoto ya baadhi ya viongozi waliohakikiwa kutokamilisha au kufanya uhaulishaji wa mali walizoziuza au walizozinunua kutoka kwa watu wengine. Hivyo, wito unatolewa kwa viongozi kuhakikisha wanakamilisha uhaulishaji wa mali zao ili kuepusha uwezekano wa kutokuwepo au kutokupatikana kwa taarifa sahihi za mali na madeni ya viongozi husika.

Kwa upande wa malalamiko yanayohusiana na uvunjaji wa maadili

kutoka kwa wananchi, Tume ya Maadili imeendelea kutekeleza kazi hiyo ambapo kwa mwaka huu wa utekelezaji 2019/2020 jumla ya malalamiko 20 yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kwa mwaka 2016/2017 malalamiko 4 yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kwa mwaka 2017/2018 malalamiko 6 yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kwa mwaka 2018/2019 malalamiko 13 yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Malalamiko haya yamejikita katika maeneo ya matumizi mabaya ya madaraka, udhalilishaji wa kijinsia, ubadhirifu wa mali za umma, uonevu, upendeleo katika ajira, kashfa na matumizi ya matusi na mgongano wa kimaslahi.

Kadhalika, kwa viongozi ambao wamechelewa ama kushindwa kuwasilisha fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni, Tume ya Maadili imepokea maelezo kutoka kwa viongozi hao na hatua muafaka zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Katika dunia ya sasa, vyombo vya habari vimekuwa na mchango mkubwa katika kufikisha taarifa mbalimbali kwa jamii. Katika kulifanyia kazi hili, Tume ya Maadili imeendelea kuvitumia vyombo vya habari vya Serikali, binafsi na redio jamii katika kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa viongozi na wananchi kuzingatia maadili katika maisha yao ya kila siku. Njia mbalimbali za kuelimisha zimetumika ili kuhakikisha Viongozi na Wananchi kwa ujumla wanapata elimu sahihi ya dhana nzima ya maadili. Miongoni mwa njia hizo ni maigizo mbalimbali, vipindi vya redio na televisheni, makala, vipeperushi na kupitia mabanda ya maonesho. Kadhalika, Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu pamoja na Kongamano la Kitaifa la Utawala Bora yaliyofanyika tarehe 16/12/2019 katika ukumbi wa mikutano wa Sheikh Idriss Abdul Wakil – Kikwajuni. Maadhimisho hayo yamekuwa ni njia muhimu sana katika kupeleka elimu ya maadili kwa viongozi na wananchi.

Katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwa Tume ya Maadili, kumekuwa na mafanikio ambayo kwa njia moja au nyengine yamechangiwa na Uongozi imara wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo basi, nimalizie kwa kutoa shukrani zangu za dhati na kipekee kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein. Shukrani hizo zinatokana na jitihada zake za kuimarisha Utawala Bora nchini katika maeneo ya uwajibikaji na kuimarisha maadili kupitia Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na taasisi nyengine za Utawala Bora. Vilevile, ninamshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuendelea kusimamia vyema utendaji wa shughuli za Serikali na kumshauri Mhe. Rais katika mambo mbalimbali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Pili, namshukuru kwa dhati Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman, pamoja na viongozi wote wa Wizara kwa mwongozo, ushauri na msaada waliotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili.

Tatu, ninawashukuru Makamishna wa Tume ya Maadili, Mhe. Sebtuu Mohammed Nassor na Mhe. Said Bakari Jecha, Katibu wa Tume ya Maadili, Nd. Asma Hamid Jidawy pamoja na watendaji wote wa Tume ya Maadili kutokana na utendaji wao uliotuwezesha kupata mafanikio tuliyoyafikia katika kipindi hiki cha miaka minne tangu kuanzishwa kwake.
Mwisho kabisa, niendelee kutoa wito kwa Viongozi wa Umma na Wananchi wote waendelee kutoa ushirikiano ambao utaiwezesha Tume ya Maadili kutekeleza majukumu yake kikamilifu ili hatimaye kufikia lengo la kuimarisha Utawala Bora katika nchi yetu.

Kwa heshima, naomba kuwasilisha.

**Assaa Ahmad Rashid**

**Mwenyekiti**
**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

***'Fuata Maadili, Tuimarishe Utawala Bora'.***

## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya mwaka 2015 imepewa mamlaka ya kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma. Mamlaka hayo yanajumuisha kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na Viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015 imeweka viwango vya maadili kwa viongozi wa umma ambavyo wanapaswa kuvizingatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa umma. Sheria hiyo imeanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Tume ya Maadili) ambayo imepewa jukumu la kuisimamia kwa lengo la kuimarisha maadili kwa viongozi wa umma.

Kutungwa na kupitishwa kwa Sheria hii ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuimarisha utawala bora nchini. Taasisi nyengine zilizoanzishwa kwa lengo la kuimarisha utawala bora ni pamoja na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Utawala Bora na Tume ya Haki za Binadam na Utawala Bora. Taasisi hizo nazo hutayarisha ripoti zao za utekelezaji kila mwaka na kuziwasilisha katika mamlaka husika.

Ripoti hii inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili katika kusimamia shughuli zake za masuala ya maadili ya viongozi wa umma. Utekelezaji huu ni kwa mujibu wa Mpangokazi wa Tume ya Maadili wa mwaka wa fedha 2019/2020, Mipango Mikuu ya Kitaifa ikijumuisha Dira ya Maendeleo ya 2020, MKUZA III na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020.

## 1.1 DIRA

Dira ya Tume ya Maadili ni *"Kuwa na jamii yenye kufuata maadili"*

## 1.2 DHAMIRA

Dhamira ya Tume ya Maadili ni *"Kukuza tabia na vitendo vyenye kufuata maadili kwa Viongozi wa umma kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria".*

## 1.3 MAADILI YA MSINGI

Utendaji kazi wa Tume ya Maadili umejengwa kwa kuzingatia misingi ya maadili ifuatayo ambayo inawaongoza watumishi wake:

(a) **Uadilifu:** Kufanya kazi kwa uwazi na bila ya upendeleo;

(b) **Usiri:** kuhifadhi na kutunza taarifa zote za siri ikiwemo taarifa zinazohusiana na mali na madeni ya Viongozi wa Umma;

(c) **Utaalamu:** Kusimamia sheria ya Maadili ya Viongozi kwa umakini na uaminifu kwa kutumia umahiri, uweledi, na utaalamu unaohitajika;

(d) **Uwajibikaji:** Kuimarisha uwajibikaji wa watumishi na wahusika wengine wa Tume; na

(e) **Kufanya kazi kwa mashirikiano:** Kukuza na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa watumishi ili kuwezesha utendaji wa kazi za Tume kwa ufanisi.

## 1.4 LENGO KUU

Lengo kuu la Tume ya Maadili ni *"Kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar"*

## 2.0 MUUNDO WA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili inaundwa na Mwenyekiti na Makamishna wawili (wa muda) ambao wanateuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mwenyekiti anasimamia kazi na anatekeleza majukumu na mamlaka ya Tume ya Maadili. Kadhalika, Tume ya Maadili ina Katibu ambaye anateuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katibu wa Tume anasimamia kazi za kiutawala za kila siku na anawajibika kwa Tume. Kadhalika, Tume ya Maadili ina Afisa Mdhamini ambaye anaratibu shughuli za Tume ya Maadili kwa upande wa Ofisi ya Tume ya Maadili, Pemba. Aidha, Tume ya Maadili ina watumishi wa fani nyengine tofauti kwa kuzingatia muundo wake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Muundo wa Tume ya Maadili ni kama unavyoonekana kwenye ***Kiambatanisho Nambari 1***.

## 2.1 IDARA ZA TUME YA MAADILI

Tume ya Maadili ina Idara mbili; Idara ya Maadili ya Viongozi na Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu pamoja na Ofisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Pemba. Idara ya Maadili ya Viongozi inajumuisha Sehemu ya Usajili na Kumbukumbu na Sehemu ya Maadili na Uchunguzi. Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu inajumuisha sehemu ya Utawala na Rasilimali Watu na Sehemu ya Mipango, Sera na Utafiti. Aidha, Tume ya Maadili ina vitengo vitano ambavyo ni: Fedha na Uhasibu, Huduma za Sheria, Uhusiano na Elimu kwa Umma, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Kitengo cha Ununuzi. Ofisi ya Tume ya Maadili Pemba inajumuisha sehemu ya Usajili na Kumbukumbu na sehemu ya Maadili na Uchunguzi.

## 2.2 WATUMISHI WA TUME YA MAADILI

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, Tume ya Maadili ina watumishi 23 ambao wako katika fani za Sheria, Mipango, Utunzaji wa kumbukumbu, Utumishi, Utawala, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uhusiano na Elimu kwa Umma, Ualimu, Ununuzi na Uhasibu. Kati ya watumishi hao 24, watumishi 12 ni wanawake na 12 ni wanaume. Tume ya Maadili katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa Watendaji, imepata wafanyakazi wapya watano (5) kutoka katika Taasisi tofauti. Watendaji hawa wamehamishiwa Tume ili kukidhi mahitaji ya Tume ya Maadili kwa mujibu wa muundo wa Tume ya Maadili. Aidha, Tume ina watumishi wawili (2) ambao wameazimwa kutoka taasisi za Serikali. Tume itaendelea kuongeza watendaji wenye fani na uzoefu katika maeneo mbalimbali ili kukabiliana na kasi ya utendaji wa kazi zake. Idadi ya Watumishi na viwango vyao vya elimu ni kama inavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 1.***

**Jadweli Nambari 1: Idadi ya Watumishi wa Tume ya Maadili na Viwango vyao vya Elimu.**

| **CHETI/FORM II** | | **STASHAHADA** | | **STASHAHADA YA JUU** | | **SHAHADA** | | **STASHAHADA YA UZAMILI** | | **SHAHADA YA UZAMILI** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | **JUMLA** |
| 1 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 1 | 4 | 5 | **24** |
| | 1 | | | | | | | | | 1 | | **2** |

## 2.3 MAJUKUMU YA TUME YA MAADILI

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Maadili ina majukumu yafuatayo:

(a) Kupokea na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni ambalo limetolewa na Kiongozi wa Umma;

(b) Kupokea tuhuma na taarifa za uvunjaji wa maadili kutoka kwa wananchi;

(c) Kufanya uchunguzi juu ya madai au tuhuma za uvunjaji wa maadili kwa kiongozi yeyote wa Umma;

(d) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia madai yote yanayohusu uvunjaji wa maadili katika chombo cha umma;

(e) Kupokea na kuchunguza jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linapelekea tuhuma ya moja ya mambo yafuatayo kuwa limetokea au linaweza kutokea:

   (i) Kitendo kinachopelekea uvunjaji wa maadili;

   (ii) Kitendo kinachopelekea kuruhusu, kushawishi au kusababisha uvunjaji wa maadili;

(f) Kuchunguza mwenendo wa kiongozi yeyote wa umma ambao kwa maoni ya Tume, unapelekea au unachangia uvunjaji wa maadili;

(g) Kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu madai yoyote ya uvunjaji wa Maadili dhidi ya Kiongozi wa Umma;

(h) Kutoa uamuzi wa uvunjaji wowote wa maadili;

(i) Kusaidia taasisi yoyote ya Serikali yenye jukumu la kutekeleza Sheria katika kufanya uchunguzi wa kosa la uvunjaji wa maadili;

(j) Kutokana na maombi ya mtu au taasisi yoyote, kushauri au kusaidia mtu au taasisi yoyote namna ambavyo kiongozi au taasisi hiyo inavyoweza kuepukana na uvunjaji wa maadili;

(k) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa maadili;

(l) Kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Tume linastahili kufanyiwa uchunguzi;

(m) Kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kuhusiana na maadili ya Viongozi;

(n) Kufanya uhakiki wa moja kwa moja kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni lililowasilishwa kwa mujibu wa sheria; na

(o) Kufanya kazi nyengine zozote ilizopewa na Sheria ya Maadili ya Viongozi au Sheria nyenginezo.

## 2.4 MAMLAKA NA UWEZO WA TUME YA MAADILI

Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake, Tume ya Maadili imepewa mamlaka na uwezo wa:-

(a) Kumuidhinisha afisa wa Tume kufanya uchunguzi wa tuhuma ya uvunjaji wa maadili (kif. 13(1)(a)).

(b) Kumtaka mtu yeyote kutoa kumbukumbu na nyaraka zozote zinazohusiana na tuhuma zinazofanyiwa uchunguzi (kif. 13(1)(b)).

(c) Kumtaka mtu yeyote kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuhojiwa kuhusiana na jambo lolote linaloshughulikiwa na Tume katika uchunguzi wa tuhuma za uvunjaji wa maadili

(kif.13(1)(c)).

(d) Kumtaka Kiongozi wa Umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni alililoliwasilisha (kif.16A).

(e) Kushirikiana na taasisi au mtu yeyote katika uchunguzi wa madai au tuhuma za uvunjaji wa Sheria ya Maadili (kif. 14(1)).

(f) Kuchunguza Akaunti ya Kiongozi wa Umma (kif.37(1)).

(g) Kuwasilisha maamuzi yake kwenye mamlaka husika (kif. 27(1)).

## 3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2019/2020

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea na kusajili Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(b) Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

(c) Kufanya uhakiki wa Taarifa za Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;

(d) Kupokea na kufanya uchunguzi wa tuhuma na malalamiko ya ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) Kujenga uelewa kwa Wananchi na Viongozi wa Umma Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa Maadili ya Viongozi wa Umma;

(f) Kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binadamu;

(g) Kuwapatia mafunzo ya kitaalam Watumishi wa Tume ya Maadili; na

(h) Kukuza na kuimarisha ushirikiano na uhusiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

## 4.0 UTEKELEZAJI HALISI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2019/2020

Katika mwaka huu wa utekelezaji, Tume ya Maadili imeweza kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo: -

### 4.1 TAMKO LA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Kila kiongozi wa umma anatakiwa kujaza na kuwasilisha Tume ya Maadili, Fomu ya Tamko la Mali na Madeni. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Fomu ya Tamko huwasilishwa Tume ya Maadili katika hali kuu tatu; kila ifikapo mwezi wa Disemba ya kila mwaka, ndani ya siku thelathini (30) baada ya kiongozi wa umma kushika madaraka au wadhifa wa uongozi na mara tu baada ya kiongozi wa umma kumaliza muda wa kushika madaraka au wadhifa wa uongozi. Kwa mujibu wa Sheria ya Maadili, kiongozi anayepaswa kujaza Fomu ya Tamko la Rasilimali na Madeni sharti awe ametajwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Katika hatua nyengine, mabadiliko ya Jadweli la Kwanza la Sheria ya Maadili yamefanyika kwa kuongeza na kupunguza baadhi ya Viongozi. Marekebisho hayo yataanza kutumika na kufanyiwa kazi ifikapo mwezi Disemba, 2020. (***Kiambatanisho Nambari 2 kinahusika***)

Kadhalika, Fomu ya Tamko la Mali na Madeni imefanyiwa marekebisho kwa lengo la kupata taarifa zaidi za kiongozi ambazo hazikuwa zikipatikana katika Fomu ya awali. Marekebisho hayo yameshapitishwa na Baraza la Mapinduzi na yanatarajiwa kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi katika kikao chake kinachofuata.

### 4.1.1 Uchapishaji na Usambazaji wa Fomu ya Tamko la Mali na Madeni

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya fomu za Tamko la Mali na Madeni 2,600 zilichapishwa na kusambazwa kwa viongozi kupitia mikutano mbalimbali ya viongozi wa umma iliyofanyika Unguja na Pemba. Aidha, fomu hizo zilipatikana katika tovuti ya Tume ya Maadili kupitia **www.ethicscommission.go.tz** ambapo baadhi ya viongozi waliweza kuzipata kupitia tovuti hiyo, kuzijaza na kuziwasilisha katika ofisi za Tume ya Maadili Unguja na Pemba. Fomu hizo pia ziliwasilishwa katika makao makuu ya kila Wizara na Taasisi husika ili viongozi waliokuwa hawakuhudhuria katika mikutano ya utoaji wa elimu waweze kuzipata kwa urahisi. Matarajio ya Tume ya Maadili ni kuendelea kuwaomba viongozi wa umma watumie njia ya kupata fomu kupitia tovuti ya Tume ya Maadili ili Serikali iweze kupunguza gharama za uchapishaji na usambazaji wa Fomu za Tamko la Mali na Madeni.

### 4.1.2 Uchambuzi wa Fomu

Kwa mujibu wa Mpangokazi wa mwaka 2019/2020, Tume ya Maadili ilikadiria kupokea jumla ya fomu 2,500 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 jumla ya fomu 2,245 zilipokelewa. Pamoja na upokeaji huo, utaratibu wa kupokea fomu kutoka kwa viongozi waliochelewa na waliopata uteuzi mpya baada ya tarehe 31 Disemba 2019 uliendelea. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Tume ya Maadili ilipokea jumla ya Fomu za viongozi 2,325 sawa na asilimia 93 ya shabaha ya fomu 2,500. Kumekuwa na ongezeko la idadi ya Fomu zilizopokelewa ikilinganishwa na fomu zilizopokelewa kwa mwaka uliopita 2018/19 (1,702. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 37.


Kati ya Fomu hizo (2,325), Fomu zilizowasilishwa ndani ya muda ni 2,245 (ikilinganishwa na 1,676 za mwaka 2018/19) na uteuzi wa viongozi wapya 27. Viongozi waliowasilisha fomu nje ya muda ni 53 kwa mwaka 2019/2020, ikilinganishwa na viongozi 26 kwa mwaka 2018/2019.

Muhtasari wa uwasilishaji wa fomu kiidadi ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 2 na Mchoro Nambari 1.***

**Jadweli Nambari 2: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu**

| **MAELEZO** | **2016/2017** | **2017/2018** | **2018/2019** | **2019/2020** |
|---|---|---|---|---|
| MAKADIRIO | 1,600 | 1,650 | 1,650 | 2,500 |
| FOMU ZILIZOWASILISHWA | 1,620 | 1,664 | 1,702 | 2,325 |
| ZIADA/(UPUNGUFU) | 20 | 14 | 52 | (172) |
| ASILIMIA - UWASILISHAJI | 101 | 101 | 103 | 93 |
| NDANI YA MUDA | 1,479 | 1,639 | 1,676 | 2,245 |
| WALIOCHELEWA | 141 | 25 | 26 | 53 |
| ASILIMIA - WALIOCHELEWA | 9 | 2 | 2 | 2 |

**Mchoro Nambari 1: Muhtasari wa Uwasilishaji wa Fomu**



### 4.1.3 Kutangaza Majina ya Viongozi wa Umma katika Gazeti Rasmi la Serikali

Kwa mujibu wa Kifungu cha 22(3) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, majina ya Viongozi wa Umma waliowasilisha fomu yalichapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali katika Tangazo la Kisheria Nambari 6 la Mwaka 2020. Majina hayo yanajumuisha Viongozi wa Umma waliowasilisha Fomu zao.

### 4.1.4 Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Taarifa za Viongozi Wasiojaza Fomu

Tume ya Maadili ilichukua juhudi maalum za kuwabaini na kujiridhisha juu ya kuwepo kwa viongozi ambao kwa makusudi hawakujaza Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Baadhi ya viongozi hao waliitwa mbele ya Tume kwa ajili ya kujieleza kabla ya kuchukuliwa hatua muafaka. Aidha, viongozi wengine waliowasilisha Fomu nje ya muda walitakiwa kutoa maelezo ya sababu za kushidwa kuwasilisha Fomu ndani ya muda uliowekwa kisheria. Uchambuzi wa maelezo yaliyowasilishwa yanaendelea kufayiwa kazi.

## 4.2 MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Mfumo wa kielekroniki kwa ajili ya usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma umeendelea kuimarishwa kwa lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji wa kazi. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, uingizaji wa Taarifa za Mali na Madeni ya viongozi umeendelea kama kawaida. Mfumo huu kwa sasa una uwezo wa kutoa barua iliyosainiwa yenye kuthibitisha kupokelewa kwa Fomu ndani ya muda na nje muda. Aidha, mfumo una uwezo wa kutoa orodha ya viongozi wote waliowasilisha Fomu za Tamko la Mali na Madeni na hivyo kurahisisha kazi ya uchapishaji wa orodha hiyo katika Gazeti Rasmi la Serikali kama Sheria ya Maadili inavyoelekeza.

Juhudi zaidi zitaendelea kuchukuliwa katika kuhakikisha taarifa za viongozi zinaendelea kuimarishwa kwa kuingiza taarifa zao zinazotokana na mabadiliko ya taarifa za viongozi husika, kutokana na sababu tofauti zikiwemo za uteuzi, kustaafu, kumaliza muda na mabadiliko ya kawaida ya nafasi za uongozi.

Katika kuhakikisha uimara na ufanisi wa mfumo huu, vifaa vyenye thamani ya Tshs. 50,000,000 vimenunuliwa kwa ajili ya Ofisi za Tume ya Maadili Pemba. Fedha hizi zimepatikana kupitia Mradi wa Serikali Mtandao (E-government). Kufungwa kwa vifaa hivyo kutawezesha mfumo huo kuwa rahisi kutumika kwa watendaji wa Tume ya Maadili waliopo katika ofisi ya Tume ya Maadili Pemba. Hii itarahisisha kubadilishana taarifa kwa njia ya mfumo wa kielektroniki kwa watendaji wa Tume ya Maadili walioko Unguja na Pemba.

Mfumo huu wa kielektroniki utakapokamilika utaiwezesha Tume ya Maadili kuhifadhi taarifa za viongozi kwa ufanisi zaidi ikiwa ni sehemu ya msingi ya kazi yake ya kuhifadhi taarifa za viongozi wa umma. Pia, utarahisisha utekelezaji wa majukumu yake katika uandaaji wa ripoti na taarifa, kufanya uchunguzi, uhakiki na utoaji wa takwimu zinazohusiana na viongozi wa umma. Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni unashughulikiwa na kusimamiwa kwa ushirikiano baina ya watendaji wa Tume ya Maadili katika Kitengo cha TEHAMA na Idara ya Serikali Mtandao.

### 4.3 UHAKIKI WA TAARIFA ZA MALI NA MADENI YA VIONGOZI WA UMMA

Kazi ya uhakiki wa taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma ni miongoni mwa kazi ya msingi ya Tume ya Maadili kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 12(1)(n) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uhakiki huu unahusiana moja kwa moja na taarifa zilizojazwa kwenye Fomu ya Tamko la Mali na Madeni kwa viongozi husika ili Tume ya Maadili iweze kujiridhisha na usahihi wa taarifa zilizotolewa. Kazi hii ya

uhakiki hufanyika mara tu baada ya Viongozi wa Umma kuwasilisha Fomu zao za Tamko la Mali na Madeni.

Tume ya Maadili kwa uwezo iliyopewa kisheria ina uwezo wa kumtaka kiongozi yeyote wa umma kutoa taarifa au maelezo ya ziada kuhusiana na Tamko la Mali na Madeni wakati wa kazi ya uhakiki.

### 4.3.1 Uchambuzi wa Taarifa za Uhakiki

Kwa mwaka huu wa utekelezaji 2019/2020, Tume ya Maadili ilipanga kuhakiki jumla ya Viongozi 220 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Jumla ya Viongozi 135 wamehakikiwa Unguja na Pemba. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 61 ikilinganishwa na viongozi 38 katika mwaka 2016/2017, viongozi 103 katika mwaka 2017/2018 na viongozi 168 katika mwaka 2018/2019. ***(Angalia Jadweli Nambari 3 na Mchoro Nambari 2*** *inahusika).* Changamoto iliyosababisha kutokufikiwa kwa lengo la kuhakiki viongozi 220 ni kutokana na mripuko wa maradhi ya homa ya mapafu (KORONA) ambapo ilikuwa vigumu kuwafikia viongozi baada ya maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya juu ya kuepuka michanganyiko ya watu. Pamoja na changamoto hiyo, kwa sasa Tume ya Maadili inajipanga vyema kuhakikisha idadi kubwa ya viongozi inafikiwa katika kazi hii ya uhakiki. Miongoni mwa hatua hizo za kujipanga ambazo tayari zimechukuliwa ni kuongeza watumishi. Aidha, katika mwaka ujao wa fedha 2020/2021, gari moja itanunuliwa kwa lengo la kupunguza tatizo la usafiri hasa eneo la uhakiki.


Kwa mwaka ujao wa fedha 2020/2021 Tume ya Maadili imepanga kuhakiki Viongozi wa Umma 200.

**Jadweli Nambari 3: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma hadi mwaka 2019/2020**

| MWAKA | VIONGOZI WALIOPANGWA KUHAKIKIWA | UTEKELEZAJI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 56 | 38 | 68 |
| 2017/2018 | 360 | 103 | 29 |
| 2018/2019 | 120 | 168 | 140 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 220 | 135 | 61 |

**Mchoro Nambari 2: Uhakiki kwa Viongozi wa Umma kwa mwaka 2018/2019**




Kazi ya uhakiki kwa mwaka huu wa fedha 2019/20 ilihusisha Makamishna kutoka Taasisi mbalimbali, Wakurugenzi wa Idara, Wakurugenzi Manispaa, Halmashauri, Wasaidizi Wakurugenzi, Mahakimu wa Mkoa na Wilaya, Wahasibu Wakuu na Wakaguzi Wakuu wa Ndani. Baada ya kuchambua ripoti za kiongozi mmoja mmoja, imebainika kuendelea kuwepo changamoto ya uhaulishaji wa mali zinazohamishika na zisizohamishika. Hali hii imepelekea kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa mali zenye majina yao. Tangu kuanzishwa kwa Tume ya Maadili miaka minne iliyopita na kuanza kazi ya uhakiki, suala hili la hatimiliki za mali za viongozi limeonekana kuwa tatizo sugu. Miongoni mwa nyaraka hizo zilizokosekana wakati wa kazi hii ya uhakiki ni kadi za umiliki wa vyombo vya moto, hatimiliki za nyumba, majengo, mashamba, viwanja, mashine na mitambo. Katika mazingira haya, wito unatolewa kwa viongozi kuhakikisha wanakamilisha utaratibu wa uhaulishaji ili kuiwezesha Tume ya Maadili kuziorodhesha katika Fomu ya Tamko la Mali na Madeni na kuzitambuwa mali halisi za viongozi

wanazomiliki. Hatua hii itahakikisha kuwepo kwa kumbukumbu sahihi za taarifa za mali zao katika Daftari la Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni.

Aidha, katika utekelezaji wa mwaka 2019/2020, Tume ya Maadili ilikusudia kufanya kazi ya uhakiki kwa viongozi wenye mali Tanzania Bara. Hata hivyo, kutokana na mripuko wa maradhi ya homa ya mapafu (KORONA) shughuli hii haikutekelezwa. Ni matarajio ya Tume ya Maadili kuwa kazi ya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wenye mali upande wa Tanzania Bara itafanyika mwaka ujao wa fedha 2020/2021.

## 5.0 KUPOKEA NA KUFANYA UCHUNGUZI WA TUHUMA NA MALALAMIKO YA UKIUKWAJI WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi imepewa mamlaka na uwezo wa kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko, tuhuma, madai au taarifa za ukiukwaji wa maadili ya Viongozi (Kifungu cha 12(1)(b)-(f) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma).

Tume ya Maadili katika kipindi cha mwaka 2019/2020, ilipokea na kuyafanyia kazi jumla ya malalamiko 20 dhidi ya Viongozi wa Umma, ikilinganishwa na malalamiko 13 katika mwaka 2018/2019. Sehemu kubwa ya malalamiko hayo ilihusiana na matumizi mabaya ya madaraka. Hata hivyo, malalamiko mengine yalihusiana na ubadhirifu wa mali za umma, udhalilishaji wa kijinsia, uonevu, upendeleo katika ajira, kashfa na matumizi ya matusi na mgongano wa kimaslahi. ***Jadweli Nambari 4*** inahusika.

**Jadweli Nambari 4: Malalamiko yaliyopokelewa hadi 2019/2020**

| S/N | Malalamiko | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Malalamiko yaliyopokelewa na Tume | 3 | 6 | 10 | 17 |
| 2 | Malalamiko yaliyopelekwa Taasisi nyengine | 1 | 0 | 3 | 3 |
| | **Jumla ya Malalamiko yaliopokelewa** | **4** | **6** | **13** | **20** |

## 5.1 Uchambuzi wa Malalamiko

Malalamiko tisa (9) kati ya ishirini (20) yanahusiana na matumizi mabaya ya madaraka. Kati ya malalamiko hayo moja linahusiana na kesi ya madai na hivyo lipo Mahakamani na yaliyobaki uchunguzi wake unaendelea na mara tu utakapokamilika wahusika wataitwa mbele ya Tume kwa ajili ya kutoa maelezo ya utetezi wao. Kwa upande mwengine, malalamiko matatu (3) kati ya 20 yanahusiana na mgongano wa kimaslahi ambapo moja kati ya hayo uchunguzi wake bado unaendelea na malalamiko mawili uchunguzi wake umefungwa baada ya uchunguzi wa awali kukamilika na Tume ya Maadili kujiridhisha kuwa malalamiko hayo mawili yaliyofunguliwa hayahusiani na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Tume ya Maadili imepewa uwezo kisheria kupitia kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kufanya uchunguzi wa awali kuhusu malalamiko yanayowasilishwa. Katika uchunguzi wa awali kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa, Tume ya Maadili ilibaini kuwa lalamiko moja (1) kati ya 20 halikuwa na ushahidi na hoja za msingi ingawa kiongozi anaelalamikiwa alishauriwa kuzingatia na kufuata maadili ya viongozi wa umma kama yalivyobainishwa katika Sheria ya Maadili ya viongozi.

Baada ya kufanyika kwa uchunguzi wa awali kuhusu malalamiko mengine saba (7) kati ya 20 yaliyowasilishwa, Tume ya Maadili bado inaendelea na uchunguzi baada ya hapo awali kusitisha shughuli za

kukutana ana kwa ana viongozi pamoja mashahidi kufuatia agizo la Serikali la kila taasisi kuchukua hatua za kujikinga na maambukizi ya virusi vya KORONA. Malalamiko yaliyowasilishwa Tume ya Maadili yamehusisha watendaji wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za SMZ, Wateule wa Mawaziri na Viongozi wa Serikali za Mitaa.

Kupitia programu zake za utoaji wa elimu, Tume ya Maadili itazidi kuendelea kutoa elimu kwa umma ili wananchi waweze kuwasilisha malalamiko yao. Kadhalika, elimu zaidi itatolewa kwa Viongozi ili kufuata masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kupunguza malalamiko ya ukiukwaji wa Maadili ya Viongozi wa Umma.

## 6.0 KUJENGA UELEWA KWA WANANCHI NA VIONGOZI WA UMMA UNGUJA NA PEMBA KUHUSU MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili inawajibu wa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa Maadili ya viongozi wa umma kama Kifungu cha 12(1)(k) cha Sheria ya Maadili kinavyoeleza. Njia mbalimbali zimetumika ili kuhakikisha elimu ya maadili inawafikia viongozi na wananchi kwa ujumla. Kuongezeka kwa uelewa juu ya dhana nzima ya maadli, itasaidia kuimarisha utawala bora nchini na jamii kutoa viongozi wenye kuzingatia umuhimu wa maadili. Mikutano ya utoaji wa elimu kwa viongozi wa umma, watumishi wa umma na wananchi ilitolewa katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Kwa upande mwengine, vipindi vya elimu na matangazo kupitia vyombo mbalimbali vya habari viliandaliwa na kurushwa hewani. Vilevile, machapisho na vipeperushi vilitayarishwa na kusambazwa. ***Jadweli Nambari 5*** *inahusika.*

### 6.1 Mikutano na Viongozi wa Umma

Tume ya Maadili kwa mujibu wa Mpangokazi wake wa mwaka 2019/2020, ilipanga kufanya mikutano 50 ya viongozi wa umma. Walengwa ni viongozi wote kutoka katika Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma. Jumla

ya mikutano yote 50 iliyopangwa ilifanyika, ambapo mikutano 33 ilifanyika Unguja na 17 ilifanyika Pemba. Mada zilizowasilishwa katika mikutano hiyo ni:

a) Mgongano wa Kimaslahi katika Utumishi wa Umma; na
b) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015 na marekebisho yake.

Pamoja na mikutano hiyo, Tume ilipata mialiko kutoka Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuelimisha watumishi wao juu ya dhana nzima ya maadili. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Shirika la Nyumba Zanzibar, Wapiganaji wa Vikosi vya SMZ, Wahariri wa Vyombo vya Habari, Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

### 6.2. Mikutano ya Wananchi na Wanafunzi

Tume ya Maadili ilifanya mikutano na wananchi pamoja na makundi mbalimbali. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, miongoni mwa wananchi waliopatiwa elimu ya maadili ni pamoja na wananchi wa Shehia ya Nungwi na Michamvi kwa Unguja na Shehia ya Uweleni na Kizimbani kwa Pemba. Kwa upande mwengine, wanafunzi wa Skuli 4 wamepatiwa elimu ya maadili. Skuli hizo ni Mahonda na Unguja Ukuu kwa Unguja na Madungu na Chuo cha Kiislam kwa Pemba.

Kadhalika, Tume ya Maadili iliandaa na kufanya mikutano mitatu. Mmoja kwa wananchi wa Vitongoji Pemba, mwengine kwa wananchi wa Michamvi Unguja na Wasanii wa kikundi cha JUFE. Lengo la mikutano hiyo ni kuitambulisha Tume ya Maadili na kutoa elimu ya maadili kwa wananchi na makundi mbalimbali. Mada mbili zilizowasilishwa katika mikutano hiyo ni:

a) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015; na
b) Umuhimu wa kuimarisha Maadili.

**Jadweli Nambari 5:**
**Mikutano ya Viongozi, Wananchi na Wanafunzi waliopatiwa Elimu ya Kukuza Maadili**

| Nam. | AINA YA KUNDI | IDADI YA MIKUTANO | MAENEO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mikutano ya Viongozi na Watumishi wa Umma | 54 | Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma |
| 2 | Mikutano ya Wananchi na Wanafunzi | 10 | Shehia ya Nungwi, Shehia ya Michamvi, Wananchi wa Michamvi, Shehia ya Uweleni, Shehia ya Kizimbani, Wananchi wa Vitongoji, Skuli ya Mahonda, Skuli ya U/Ukuu, Skuli ya Madungu, Chuo cha Kiislam Pemba |
| 3 | Mikutano na Wahariri na Wasanii | 2 | Wahariri - Unguja na Wasanii wa JUFE Pemba |

### 6.3 Utayarishaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu na Matangazo kupitia Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuelimisha umma juu ya mambo mbalimbali yakiwemo masuala ya maadili. Tume ya Maadili haikuwa nyuma katika kuhakikisha viongozi na jamii kwa ujumla wanafikiwa katika kuwapatia habari na elimu kuhusu umuhimu wa maadili. Katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka 2019/2020, Vipindi 31 vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia vituo mbalimbali vya Redio na Televisheni. Vituo vilivyotumika kurusha vipindi hivyo ni Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni.

Katika vipindi hivyo mada tofauti zilizungumzwa zikiwemo; Kazi na Majukumu ya Tume ya Maadili, Jukumu la Wananchi na Jamii katika Kusimamia na Kuhakikisha Viongozi wanasimamia na kufuata maadili na Wajibu wa Viongozi wa Umma katika Kuimarisha Maadili.

### 6.4 Utoaji wa Machapisho na Matangazo

Katika kuhakikisha kuwa jamii inafikiwa kwa kupewa elimu na taarifa zinazohusiana na kazi na majukumu ya Tume ya Maadili ya Viongozi,

jumla ya kalenda 3,000 zilichapishwa na kusambazwa katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar yaliyofanyika tarehe 4 Februari, 2020.

Kadhalika, Tume ya Maadili iliandaa na kurusha hewani matangazo mbali mbali yaliyotolewa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) - Redio na Televisheni na kupitia Gazeti la Zanzibar Leo. Katika matangazo hayo Viongozi walielimishwa juu ya kutambua wajibu wao na kutekeleza masharti yaliyomo katika Sheria Namba 4 ya Mwaka 2015. Miongoni mwa masharti ya Sheria hiyo ni kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni na Mienendo ya viongozi wa umma katika kutekeleza na kusimamia majukumu yao.

## 7.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI

Kila ifikapo tarehe 10 Disemba ya kila mwaka, Zanzibar huadhimisha Kitaifa Siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Siku hii imetokana na Siku mbili tofauti – ambazo ni Siku ya Kupinga Rushwa Duniani inayoadhimishwa kila ifikapo tarehe 9 Disemba ya kila mwaka na Siku ya Haki za Binadamu Duniani huadhimishwa kila ifikapo tarehe 10 Disemba ya kila mwaka. Kwa mnasaba huo Tanzania imeamua kuadhimisha kwa pamoja Siku hizo tarehe 10 Disemba ya kila mwaka.

Kwa mwaka 2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuadhimisha siku hii tarehe 16 Disemba, 2019 katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil, Kikwajuni Mjini Unguja. Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein.

Taasisi zinazohusika moja kwa moja na usimamizi wa Maadili na Haki za Binaadamu ni tano (5) nazo ni: Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Utawala Bora na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kupitia siku hii ya maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binaadamu, taasisi hizi hufanya shughuli mbali mbali

ikiwemo kuratibu matukio yenye mnasaba na uimarishaji wa Maadili na Utawala Bora nchini.

Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka 2019 ni ***"Maadili katika Utumishi wa Umma ni msingi wa Utawala Bora, haki za Binadamu na Mapambano dhidi ya Rushwa"***.

Madhumuni ya maadhimisho ya Siku ya Maadili ni kuongeza uelewa mpana zaidi wa viongozi na wananchi juu ya dhana ya Utawala Bora na misingi yake ikiwemo masuala ya maadili, masuala ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi, ulinzi wa Haki za Binadamu, usimamizi wa rasilimali za umma, uwajibikaji, uwazi na uadilifu. Kuimarika kwa misingi hiyo kunasaidia wananchi kuzitambua na kupata haki za msingi, maendeleo na ustawi wa maisha, kupunguza umasikini na kukuza uchumi, kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini, kuongezeka kwa upendo na uzalendo, na kupata viongozi bora na wawajibikaji.

## 8.0 KUWAPATIA MAFUNZO YA KITAALAM WATUMISHI WA TUME YA MAADILI

Tume ya Maadili katika kuwajengea uwezo watumishi wake, imewapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi wawili, mmoja katika eneo la Utunzaji wa Kumbukumbu na mwengine udereva (Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam). Aidha katika kuhakikisha usalama wa watumishi na mali za ofisi, Tume ya Maadili imewapatia watumishi wake pamoja na walinzi mafunzo ya ndani ya kupambana na majanga ya moto. Mafunzo haya yaliendeshwa na wakufunzi kutoka Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Kwa upande mwengine, Tume ya Maadili imewapatia mafunzo ya ndani watumishi wake kuhusu Upimaji Utendaji kazi (Performance Appraisal), lengo kuu la mafunzo haya ni kuwajengea uelewa na ufahamu wa utaratibu wa kupima utendaji kazi wa mtumishi mmoja mmoja pamoja

na kutambua njia zinazotumika katika kupata nyongeza ya mshahara anayostahiki mtumishi kwa mujibu wa utendaji wake. Aidha, watumishi wa Tume ya Maadili walipatiwa mafunzo yanayohusiana na Maadili katika Utumishi wa Umma ili kuimarisha uweledi katika utekelezaji wa kazi zao.

Kadhalika, mafunzo ya Huduma ya Kwanza (First Aid) yametolewa kwa watumishi wa Tume ya Maadili ili kuwawezesha kukabiliana na dharura za kiafya pindi zinapojitokeza. Aidha, watumishi wa Tume ya Maadili wamepatiwa mafunzo ya uingizaji wa taarifa za Mali na Madeni za Viongozi wa Umma katika Mfumo wa Ki-elektroniki utakaotumika katika shughuli za usajili wa taarifa za Viongozi wa Umma. Katika robo ya nne ya mwaka, Tume ya Maadili ilipanga kupeleka watumishi wanne kupatiwa mafunzo ya Uongozi na Maadili katika Taasisi ya Kitaifa ya Uzalishaji (NIP). Kutokana na mripuko wa homa ya mapafu (KORONA) shughuli hii haikutekelezwa. Mafunzo hayo yamepangwa kutolewa katika mwaka ujao wa fedha 2020/2021.

## 9.0 KUKUZA NA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA UHUSIANO KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tume ya Maadili ilipanga kutekeleza shughuli hii kwa kushiriki katika mikutano, semina, warsha na kutembelea Taasisi zenye majukumu sawa na Tume ya Maadili. Katika kutekeleza shughuli hii, mtendaji mmoja alishiriki kikao cha mashirikiano baina ya watendaji wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya SMZ na watendaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya SMT. Hata hivyo, shughuli hii haikuweza kufanyika kikamilifu kutokana na janga la maradhi ya homa ya mapafu duniani. Matarajio ni kuwa, mara tu baada ya hali ya kawaida kurejea shughuli hii itatekelezwa kama ilivyopangwa kwa mwaka wa

fedha 2020/2021.

## 10.0 VIKAO VYA TUME

Tume ya Maadili imefanya vikao vya kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu uvunjwaji wa Maadili dhidi ya Viongozi wa umma pamoja na vikao vya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili. Vikao vinne (4) vya Tume vimefanyika katika kipindi hiki cha utekelezaji, ambapo mambo mbalimbali kuhusiana na masuala ya Tume ya Maadili na maadili ya viongozi wa umma yalijadiliwa na kutolewa uamuzi.

## 11.0 HALI YA MAPATO NA MATUMIZI

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tume iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 977,872,680 ambapo Tshs. 681,500,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tshs. 296,372,160 kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020, jumla ya Tshs. 519,098,885 sawa na asilimia 76 zilipatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tsh. 289,540,415 zilipatikana kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi sawa na asilimia 98. Aidha, Tshs. 50,000,000 zilipatikana kwa ajili ya mradi wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa taarifa za mali na madeni.

Muhtasari wa hali ya mapato na matumizi ni kama unavyoonekana katika ***Jadweli Nambari 6 na 7*** inahusika.

**Jadweli Nambari 6: Hali ya Mapato na Matumizi.**

| RUZUKU | MWAKA | KILICHOTENGWA | KILICHOPATIKANA | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| **Mshahara na Stahiki** | **2018/2019** | 212,400,000 | 212,400,000 | 100 |
| **Matumizi Mengineyo (OC)** | | 525,000,000 | 490,000,000 | 93 |
| **Jumla** | | **737,400,000** | **702,400,000** | **95** |
| **Mshahara na Stahiki** | **2019/2020** | 296,372,160 | 289,540,415 | 98 |
| **Matumizi Mengineyo (OC)** | | 681,500,000 | 519,098,885 | 76 |
| **Jumla** | | **977,872,680** | **808,639,300** | **83** |
| **Maendeleo** | | **50,000,000** | **50,000,000** | **100** |

## 12.0 VIKWAZO NA UTATUZI WAKE

Tume ya Maadili imepiga hatua na kupata mafanikio ya kuridhisha katika utekelezaji wa majukumu yake. Mafanikio hayo yanatokana na mipango na mikakati madhubuti iliyojipangia na inayosimamiwa vyema na watendaji wa Tume. Licha ya mafanikio hayo, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ipasavyo. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto na njia zilizotumika kutatua changamoto hizo:

i. Kukosekana kwa taarifa za baadhi ya viongozi wanaoteuliwa, wanaobadilishwa nafasi za uongozi, wanaostaafu au wanaohamishwa kutoka Taasisi moja kwenda nyengine. Hali hii hupelekea kukosekana kwa taarifa sahihi za viongozi hao; - Tume ya Maadili inaendelea kuwahimiza Wakuu wa taasisi kuipatia Tume taarifa za viongozi kuhusiana na uteuzi, mabadiliko, uhamisho na kustaafu katika Taasisi zao.

ii. Baadhi ya viongozi wamekuwa wazito wa kutoa taarifa za wenza wao wakati wa ujazaji wa Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Hali hii huathiri utendaji kazi wa Tume hasa katika shughuli ya uhakiki wa taarifa za mali na madeni; - Tume ya Maadili imeendelea kutoa elimu kwa viongozi wa umma kuhusiana na suala zima la uwazi na uwajibikaji. Utoaji wa taarifa za wenza unarahisisha kupatikana kwa taarifa sahihi za viongozi za mali na madeni za viongozi wa umma.

iii. Baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya Sheria za nchi pamoja na majukumu na kazi zinazofanywa na Tume ya Maadili. Hali hii inaweza kupelekea wananchi kukosa haki zao, kuwasilisha malalamiko yasiyo na msingi au katika taasisi isiyohusika, kuwasilisha malalamiko yaliyo nje ya mamlaka ya Tume; – elimu inaendelea kutolewa kwa umma kuhusu Sheria ya Maadili, majukumu na kazi za Tume pamoja na umuhimu wa kulinda maadili.

iv. Mripuko wa maradhi ya homa ya mapafu (KORONA) umeathiri utendaji kazi wa Tume ya Maadili katika robo ya tatu na ya nne. Utendaji kazi wa Tume ya Maadili unategemea zaidi mawasiliano ya ana kwa ana, hatua ambayo haikuweza kufanyika kutokana na miongozo ya wataalamu wa afya ya kupambana na maambukizi ya virusi vinavyosababisha maradhi hayo; - Kutokana na miongozo hiyo, Tume ya Maadili haikuweza kutekeleza baadhi ya shughuli kama zilivyotajwa awali na imepanga kuzitekeleza katika mwaka ujao wa fedha 2020/2021.

## 13.0 MIKAKATI YA TUME YA MAADILI KWA MWAKA 2020/2021

Tume ya Maadili imepanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mikakati ifuatayo:

i. Kuhakiki Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;

ii. Kukamilisha mfumo wa ndani wa ki-elektroniki utakaotumika katika kusajili na kuhifadhi Taarifa za Mali na Madeni;

iii. Kuongeza kasi ya uchunguzi wa malalamiko na tuhuma za ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi na kuchukua hatua za kisheria;

iv. Kujenga uwezo wa Tume ya Maadili kwa kuwapatia mafunzo maalum watumishi wake na vitendeakazi mbalimbali;

v. Kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa Wananchi na Viongozi wa Umma Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kukuza maadili; na

vi. Kukuza na kuimarisha ushirikiano na uhusiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

## 14.0 MAPENDEKEZO

Ili Tume ya Maadili iweze kufanikisha utekelezaji wa kazi na majukumu yake, inapendekeza mambo yafuatayo:

i. Viongozi waendelee kuipa Tume ya Maadili ushirikiano unaohitajika na kutoa taarifa sahihi za Mali na Madeni kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 4 ya Mwaka 2015.

ii. Serikali iingize masuala ya maadili katika mitaala ya elimu ili kuwaandaa wanafunzi kuwa viongozi bora au raia wema

wanaoweza kusimamia maadili.

iii. Kutokana na kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la uhaulishaji wa mali zisizohamishika na zinazohamishika, wito unazidi kutolewa kwa Mamlaka zinazohusika na uhaulishaji zikiwemo; Bodi ya Uhaulishaji Ardhi, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na Bodi ya Mapato Zanzibar n.k ziendelee kuwashajihisha wananchi kuhusu umuhimu wa kukamilisha taratibu za uhaulishaji wa mali zao ili kuthibitisha umiliki wa mali hizo.

## 15.0 HITIMISHO

Jukumu la kusimamia maadili ambalo Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar imepewa, limetekelezwa ipasavyo. Kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na Viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili ni miongoni mwa kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki cha utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Sheria ya Maadili Namba 4 ya Mwaka 2015, imetaja orodha ya viongozi wa umma kwa ufasaha katika Jadweli ya kwanza ya Sheria hiyo. Hivyo ni wajibu wa viongozi wote waliotajwa katika Sheria hii kuhakikisha wanaisoma na kuielewa vyema ili kujiepusha na vitendo vitakavyopelekea uvunjifu wa maadili. Usimamizi wa maadili unahusisha viongozi, wananchi na taasisi zenye majukumu yanayofanana na ya Tume ya Maadili. Ni ukweli usiopingika kuwa utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili unategemea sana ushirikiano wa karibu ukijumuisha upatikanaji wa taarifa kutoka kwa viongozi wenyewe, wananchi na taasisi za umma.

Ushirikiano unaotolewa kupitia taarifa mbalimbali, ndio chachu na

chanzo kikuu kwa Tume ya Maadili kutekeleza kazi zake za kupokea, kusajili na kuhifadhi Tamko la Mali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma. Bila ya kupatikana kwa taarifa hizo Tume ya Maadili haiwezi kufanya uhakiki wa taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa umma wala kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya uvunjaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Masuala yote hayo ya kupatikana taarifa yanategemea sana kiwango cha elimu ya maadili kinachotolewa kwa viongozi na wananchi kwa ujumla. Katika kulitekeleza hili mikutano katika ngazi na makundi mbalimbali ilifanyika Unguja na Pemba.

Ili wananchi waweze kutimiziwa mahitaji yao ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, ni lazima kuwe na viongozi bora ambao wataacha kutumikia maslahi yao binafsi na badala yake kutanguliza maslahi ya umma. Hivyo, Tume ya Maadili inaelewa wazi jukumu zima la kuimarisha kazi zake za kuelimisha umma ili jamii nzima iweze kubadilika na hatimaye kujengeka katika misingi ya kimaadili ambayo itapelekea kuwa na viongozi bora wenye kujali mahitaji ya umma.

Ripoti hii ya Nne ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili imeelezea utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/2020. Lengo la ripoti hii ni kuongeza uelewa na ufahamu kwa viongozi wa umma, wananchi, taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuhusu shughuli zilizotekelezwa na changamoto ambazo Tume ya Maadili imekabiliana nazo katika kutekeleza majukumu yake.


## 16.0 UWASILISHAJI WA RIPOTI

Ripoti hii inawasilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**, kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, leo **tarehe 25 Septemba, 2020**.

**Kwa heshima, naomba kuwasilisha.**

**ASSAA A. RASHID**
**MWENYEKITI**
**TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**ZANZIBAR.**

**Kiambatanisho Nambari 1: Muundo wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**



**Kiambatanisho Nambari 2: ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA**

**(Chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015)**

1. Rais wa Zanzibar
2. Makamu wa Kwanza wa Rais
3. Makamu wa Pili wa Rais
4. Jaji Mkuu
5. Spika, Naibu Spika na Katibu wa Baraza la Wawakilishi
6. Waziri na Naibu Waziri
7. Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali
8. Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu na Kadhi wa Mahkama ya Kadhi
9. Mufti, Naibu Mufti, Katibu wa Mufti na Naibu Katibu wa Mufti
10. Jaji wa Mahkama Kuu na Hakimu wa Mahkama wa ngazi zote
11. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi
12. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi
13. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya
14. Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu
15. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
16. Mkurugenzi wa Mashtaka na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka
17. Mtakwimu Mkuu wa Serikali
18. Mhasibu Mkuu wa Serikali na Naibu Mhasibu Mkuu wa Serikali
19. Mkemia Mkuu wa Serikali na Mfamasia Mkuu
20. Kamishna na Naibu Kamishna wa Tume, Kamisheni, Idara na Taasisi nyengine za Serikali
21. Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Ushauri, Baraza na Bodi nyengine za Taasisi za Serikali ambae ni Muajiriwa wa SMZ
22. Mshauri wa Rais, Mshauri wa Makamu wa Rais na Mshauri wa Waziri

23. Katibu wa Rais, Naibu Katibu wa Rais, Msaidizi wa Rais na Naibu Msaidizi wa Rais
24. Katibu Mtendaji, Katibu na Naibu Katibu wa Tume, Kamisheni, Baraza na Taasisi nyengine za SMZ
25. Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu na Mkuu wa Skuli wa Chuo Kikuu cha Umma
26. Mkuu wa Chuo au Taasisi ya Umma
27. Mrajis, Naibu Mrajis wa Mahkama Kuu na Mtendaji Mkuu wa Mahkama.
28. Mkurugenzi Mkuu, Naibu Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi Mtendaji, Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Mkurugenzi Mwendeshaji, Naibu Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Umma, Bodi, Wakala na Taasisi nyengine za SMZ.
29. Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Wizara, Idara na Taasisi nyengine za SMZ
30. Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi na Mkurugenzi Msaidizi wa Baraza la Mji na Mkurugenzi na Mkurugenzi Msaidizi wa Halmashauri ya Wilaya
31. Mrajis na Naibu Mrajis wa Tume, Bodi, Wakala, Baraza, Shirika la Umma na Taasisi nyengine za SMZ
32. Meneja Mkuu, Meneja na Mkuu wa Shirika la Umma Zanzibar
33. Meya, Naibu Meya, Diwani na Sheha
34. Katibu Tawala na Msaidizi Katibu Tawala wa Mkoa na Katibu Tawala na Msaidizi Katibu Tawala wa Wilaya
35. Afisa Mdhamini wa Wizara na Taasisi nyengine za SMZ
36. Mwenyekiti wa Tume, Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Ushauri, Baraza na Taasisi nyengine za SMZ
37. Katibu, Naibu Katibu wa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais na Msaidizi wa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais
38. Ofisa wa Sekretarieti wa Baraza la Mapinduzi

39. Mhasibu wa Wizara, Idara na Taasisi nyengine za Serikali
40. Mkaguzi wa Hesabu za Serikali wa Wizara, Idara na Taasisi nyengine za SMZ
41. Afisa Kodi kutoka katika Taasisi ya ukusanyaji wa mapato ya SMZ
42. Katibu wa Bodi ya Zabuni na Afisa Ununuzi wa Wizara, Idara na Taasisi nyengine za SMZ
43. Afisa Dhamana wa Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya Umma
44. Mkuu wa Idara Maalum, Naibu Mkuu wa Idara Maalum, Mkuu wa Utawala, Mkuu wa Kamandi na Mkuu wa Zoni wa Idara Maalum za Smz
45. Meneja, Meneja Msaidizi, Mkurugenzi, Mkurugenzi Msaidizi, Mkuu wa Idara, Afisa Dhamana anayeteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Ushauri, Tume, Baraza au Taasisi nyengine za Serikali
46. Katibu wa Bodi anayeteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Ushauri, Tume, Baraza au Taasisi nyengine za Serikali
47. Wateule Wengine wa Rais na Waziri